


TAARIFA YA BENDERA

Bendera ya taifa letu la Kenya lazima ipewe heshima na umuhimu unaostahili. Haifai kupeperushe bendera usiku kwani hakuna anayeweza kuiona pasipo mwangaza. Huku kupeperusha bendera usiku hudhoufisha maisha ya bendera maradufu. Wakati bendera inaposhushwa jioni, iwapo kuna mvua tandaza bendera yenyewe chini ili iweze kukauka kabisa kabla ya kuikunja.

ITIFAKI YA BENDERA

1. Iwapo bendera ya Taifa inapeperushwa, ni lazima iwe katika mlingoti mwandamizi
2. Mlingoti mwandamizi ni
 - a) Mlingoti wa juu kabisa uwe katika kundi
 - b) Mlingoti ikiwa katika mstari (mjengo ukiwa nyuma yako) mlingoti mwandamizi uko upande wa kulia wa mstari. (Ukiziangalia ni upande wa kushoto)
3. Usipeperushe kamwe bendera moja juu ya nyingine katika mlingoti mmoja, kwani kwa Kwa kufanya hivi, bendera iliyoko chini itakuwa imetekwa na bendera iliyoko juu yake.
4. Si Kawaida kupeperusha bendera mbili tofauti katika mlingoti mmoja na kwenya kimo. Au urefu sawa, kwani bendera hazipeperuki vyema wala hazitatambuliki.
5. Bendera ya taifa la KENYA huwa kipaumbele, dhidi ya bendera za kampuni ambazo Huchukua kipaumbele dhidi, ya bendera za vitengo fulani.
6. Licha ya yaliyotajwa katika ibara ya tano kuhusukuipa bendera kipaumbele hakuna Jambo lolote limeandikishwa na kuthibitishwa. Iwapo bendera nyingi zinapeperushwa Basi watu wengi huipa bendera ya jumuiya ya madola kipaumbele kishaa bendera za Mataifa mengine ya kigeni na hatimaye bendera hufuatana na mpango wa alfabeti.
7. Haifai kwa vyovyote vile kutumia bendera ya taifa la KENYA kibiashara, kuongeza nembu au alama yoyote ile
8. Daima peperusha bendera safi, na upandishe juu kabisa kwenye mlingoti.
9. Kamwe usipeperushe bendera nusu mlingoti, isipokuwa siku ya maombolezo ya kitaifa Kwa amri ya serikali.
10. Wakati bendera iliyokuwa nusu mlingoti yateremushwa ni sharti ipandishe juu hadi Mwisho wa mlingoti kisha uiteremushe chini.
11. Iwapo haiwezekani kupandisha bendera zote zilizoko na vilevile kuziteremusha kwa Wakati mmoja, basi ni bora kuipandisha bendera ya taifa mwanzo na kuziteremusha ikiwa ya mwisho baada ya zingine zote.
12. Usitumie bendera ya taifa kama kitambaa cha meza kwenye mikutano ya umma. Yafaa iwe juu, nyuma ya jukwaa.
13. Usiache mlingoti bila bendera mchana, kwani ni ishara ya kutowajibika.



MAKINI

Hakikisha kuwa bendera ya taifa yapeperushwa ikiwa wima. Rangi za bendera zafaa kufuatana kuanzia iliyoko juu ikiwa nyeusi kisha nyeupe ikifuatana na nyekundu kisha Nyupe hatimaye kijani. Ncha ya mikuki iliyo juu ya ngao ya kimaasai lazima ielekee juu